JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)

TAARIFA YA MKAGUZI NA TAARIFA ZA FEDHA ZA LESA SACCOS LTD KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2020

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika
(COASCO)
Barabara ya Hatibu
S.L.P. 761
Simu: (026) 2323265, 2321485
Mkurugenzi Mkuu (026) 2321704
Mkurugenzi wa Ukaguzi (026) 2322050
Mkurugenzi wa Fedha na Utawala (026) 2321605
Mkurugenzi wa Utafiti na Ushauri (026) 2321671
Fax Na: 0262321486
Email: info@coasco.go.tz
DODOMA
TANZANIA

MEI, 2021 ROA/LESA SACCOS LTD/2020

YALIYOMO

NA.	Maelezo	Ukurasa
1.	Maelezo ya Awali	1
2.	Taarifa za Chama	2
3.	Takwimu...	3
4.	Taarifa ya Wajumbe wa Bodi	4-9
5.	Tamko la Mkuu wa Fedha...	10
6.	Taarifa Huru ya Wakaguzi	11-14
7.	Taarifa ya Hali ya Fedha	15
8.	Taarifa ya Mapato na Matumizi	16
9.	Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji	17
10.	Taarifa ya Mtiririko wa Fedha	18
11.	Majedwali ya Ufafanuzi wa Taarifa za Fedha	19-28

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

(COASCO)

Tanzania Bara

(Lilianzishwa kwa kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na.15 ya mwaka 1982)

Kifungu cha 4(1)(a) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na.15 ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2005 kinaipa COASCO Mamlaka ya kuvikagua Vyama vya Ushirika.

Dira

Kuwa kituo cha kipekee cha utoaji huduma bora za ukaguzi na ushauri wa Vyama vya Ushirika katika Mashariki mwa Afrika.

Dhima

Daima kuendelea kutoa huduma bora ya ukaguzi na ushauri kuongeza utawala bora kwa wateja.

Miiko inayoongoza Shirika kuelekea kwenye Dira yetu na kusaidia kufanikisha Dhima yetu ni kama ifuatavyo:

(i) Kufuata maadili ya taaluma
(ii) Kuzingatia ubora na utoaji huduma haraka
(iii) Kutopendelea, Ushirikiano na Moyo kwa kufanyakazi pamoja
(iv) Elimumwendo na Uvumbuzi
(v) Kutokuwa na ubaguzi wa kijinsia

Tunafanya haya kwa:

- Kuchangia katika Usimamizi bora wa fedha za Umma kwa kuhakikisha kwamba wateja wetu wanawajibika kwa rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuboresha ubora wa huduma za Umma kwa kusaidia uvumbuzi katika matumizi ya rasilimali za Umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wateja wetu juu ya mapungufu yaliyopo katika mifumo ya utendaji;
- Kuwashirikisha wateja wetu katika mchakato na mzunguko wa ukaguzi; na
- Kuwapatia wakaguzi wetu vitendea kazi vya kutosha na vifaa vinavyowafanya wawe huru.

KAULI MBIU

Daima Kauli Mbiu yetu ni *"COASCO kwa Ukaguzi na Usimamizi bora wa Ushirika"*

TAARIFA ZA CHAMA

Wajumbe wa Bodi

1.	Eva Bosco	Mwenyekiti
2.	Gwamaka Japhari	Makamu Mwenyekiti
3.	Edwin Mwakilasile	Mjumbe
4.	Semaly Kisamo	Mjumbe
5.	Dr Oscar Rwabiyago	Mjumbe
6.	Dr Edward Machage	Mjumbe
7.	Joyce Mndambi	Mjumbe

Supervisory Committee Members

1.	Suzana Millinga	Mwenyekiti
2.	Joseph Kaiza	Mjumbe
3.	Shafii Mmile	Mjumbe

Mawasiliano

LESA SACCOS LTD
S.L.P 9123
DAR -ES- SALAAM

Benki Inayotumika

NMB PLC
Tawi la Msasani
S.L.P 33841
DAR -ES- SALAAM

CRDB Bank PLC
Tawi la Msasani
S.L.P 106263
DAR -ES- SALAAM

Wakaguzi

COASCO
S.L.P 761
DODOMA

TAKWIMU KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31.12.2020				2020	2019
A	Wanachama	Hai	Me	144	138
			Ke	98	104
		Sinzia	Me	-	-
			Ke	-	-
	Jumla			242	242
				TSHS	TSHS
B	Financial				
	Jumla ya Mali			4,908,505,084	3,731,638,632
	Mawekezo ya Wanachama (Akiba na Amana)			4,233,694,420	3,253,139,047
	Mikopo kwa Wanachama			4,580,637,240	3,394,233,944
	Mtaji tete (core capital)			369,371,569	258,692,594
	Hisa za wanachama			311,180,036	207,890,036
	Mtaji halisi wa chama (Institutional Capital)			58,191,533	50,802,558
	Jumla ya Mapato			275,048,560	53,059,700
	Jumla ya riba juu ya Mikopo			155,201,029	309,722,117
	Jumla ya Matumizi			256,644,899	293,901,107
	Wafanyakazi	Kudumu	Me	-	-
			Ke	-	-
				-	-
		MKATABA	Me	2	2
			Ke	1	1
				3	3
C	**Key Ratios:**				
(i)	**Uwiano tosheleziwa mtaji (≥ 11%)**				
	Mtaji tete/Jumla ya Mali			7.53%	6.93%
	Mtaji tete/Mawekezo ya wanachama			8.72%	7.95%
	Mtaji halisi wa chama/Jumla ya mali			1.19%	1.36%
(ii)	**Uwiano wa Ukwasi**				
	Jumla ya Ukwasi/Jumla ya mawekezo & mader muda mrefu			108%	108%
(iii)	Ufanisi wa uendeshaji/Uwiano wa ubora wa m Jumla ya Matumizi/Jumla ya Mapato			93.31%	553.91%

TAARIFA YA BODI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2020

Bodi ya inatoa taarifa yake kuhusiana na hesabu zisizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31.12.2020 ambayo inaonesha hali ya kiutendaji ya SACCOS.

UANDIKISHWAJI

LESA SACCOS iliandikishwa tarehe **7 Febuari, 2010** na kupewa namba ya usajili **DSR 1299** kwa sheria ya ushirika **Na.6** ya mwaka **2013.**

DIRA-(VISION)

Dira yetu ni kuwa moja kati ya SACCOS zinazotoa huduma bora kwa wanachama katika SACCOS za watumishi Tanzania.

DHIMA-(MISSION)

Dhimakuu ya SACCOS yetu ni kutoa huduma za kuweka akiba, hisa na amana na kutoa mikopo kwa wanachama wetu pamoja nakuinua na kustawisha hali ya uchumi na maisha yao kwa kuanzisha na kumiliki SACCOS kidemokrasia na kuchangia mtaji na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za Vyama vya Ushirika

Wajumbe wa bodi ya SACCOS ambao wameiongoza SACCOS hadi tarehe ya taarifa hii, isipokuwa pale itakapoonyeshwa vinginevyo ni:

Na	Jina	Wadhifa	Umri	Elimu/ taaluma	Uraia	Tarehe ya kuchaguliwa
1	Ndg.Eva Bosco	M'kiti	38	ADVANCED DIPLOMA IN ACCOUNTANCY	TZ	Dec 31 ,2020
2	Ndg. Gwamaka Japhari	M/M'kiti	52	MBA	TZ	Dec 31 ,2020
3	Ndg.Edwin Mwakilasile	Mjumbe	42	DIPLOMA IN LAW	TZ	Dec 31 ,2020
4	Ndg.Semaly Kisamo	Mjumbe	38	Masters-Public Policy	TZ	Dec 31 ,2020
5	Dr.Oscar Rwabiyago	Mjumbe	37	Masters-Public Health	TZ	Dec 31 ,2020
6	Dr. Edward Machage	Mjumbe	42	Masters - Public Health	TZ	Dec 31,2020
7	Ndg. Joyce Mndambi	Mjumbe	47	MBA	TZ	Dec 31,2020

Aidha SACCOS inayo pia kamati ya usimamizi iliyochaguliwa katika mkutano mkuu wa wanachama yenye wajumbe watatu (3) kama ifuatavyo:

KAMATI YA USIMAMIZI

Na	Jina	Wadhifa	Umri	Elimu/ taaluma	Uraia	Tarehe ya kuchaguliwa
1	Suzana Millinga	Mwenyekiti	38	MBA	TZ	Dec 31 ,2020
2	Joseph Kaiza	Mjumbe	50	Masters - Economics	TZ	Dec 31 ,2020
3	Shafii Mmile	Mjumbe	46	CPA (T), MBA _ Accountant	TZ	Dec 31 ,2020

UTAWALA BORA

Bodi ya LESASACCOS inajumuisha wajumbe **07 (Saba)** na hakuna mjumbe ambaye ameajiriwa kama mtendaji wa SACCOS.Bodi inao wajibu wa kusimamia shughuli za SACCOS na kuhakikisha kuwa inatambua maeneo yenye hatari kwa shughuli za SACCOS pamoja na kupanga, kuamua na kusimamia mambo muhimu ya kifedha, kupitia na kufanya tathmini za bajeti pamoja. Bodi inalo jukumu pia la kuhakikisha kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani pamoja na sera madhubuti zinakuwepo na zinafuatwa kwa kuzingatia kanuni na misingi ya utawala bora.

Kulingana na katiba ya SACCOS yetu, Bodi inapaswa kukutana angalau mara **4 au 5** kwa mwaka. Bodi imekasimu shughuli za kila siku za kiutendaji wa SACCOS kwa Meneja ambaye anasaidiana na wajumbe wengine pamoja na watendaji wawili. Meneja na watendaji hualikwa kuhudhuria vikao vya Bodi ili kuwezesha uendeshwaji wa kikao kama viungo kati ya menejimenti na Bodi.

SACCOS inaendeshwa kwa kufuata misingi na kanuni ya utawala bora. Wajumbe wa bodi wanatambua umuhimu wa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Kamati ya Bodi iliyopo ni kamati ya mikopo yenye wajumbe wafuatao

KAMATI YA MIKOPO

Na	Jina	Wadhifa	Umri	Elimu/ taaluma	Uraia	Tarehe ya kuchaguliwa
1	Ndg.Semaly Kisamo	Mwenyekiti	35	Masters- Public Policy	TZ	Dec 31 ,2020
2	Edwin Mwakilasile	Mjumbe	43	DIPLOMA IN LAW	TZ	Dec 31 ,2020
3	Dr. Oscar Rwabiyago	Mjumbe	38	Masters of Public Health	TZ	Dec 31,2020

Katika kuhakikisha utawala bora ndani ya SACCOS kamati hii ya bodi inao wajumbe wafuatao kama ilivyooneshwa hapa juu.

Kamati ya mikopo hutoa taarifa kwa Bodi na ilikutana mara **12** katika mwaka huu. Bodi nzima ilikutana mara **05**katika mwaka huu.

Aidha SACCOS pia inayo kamati ya usimamizi yenye wajumbe watatu Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, ambao huchaguliwa na kuwajibika moja kwa moja na mkutano mkuu wa wanachama wote. Kamati ilikutana mara **04** katika mwaka huu na pia ilitoa taarifa yake katika mkutano wa wanachama wote uliofanyika tarehe 11 Decemba, 2020.

MTAJI WA SACCOS

Katika mwaka huu mtaji wa SACCOS unajumuisha hisa, malimbikizo ya faida, misaada ya mali na matengo ya akiba mbalimbali za kisheria kama ifuatavyo:

Hisa- Tsh. 311,180,000/=
Malimbikizo ya faida - Tsh. 36,611,083
Matengo mbalimbali ya kisheria -Tsh. 64,741,351/=

MENEJIMENTI

Menejimenti ya SACCOS ipo chini ya Meneja ambaye anaongoza idara ya fedha na afisa mikopo ambaye anaongoza idara ya mikopo.

WANAHISA

Wanahisa wa SACCOS ni wanachama wote ambao idadi yao ni 227, thamani ya hisa zote ni shilling 311,180,000/=na thamani ya hisa moja ni shilling 10,000/=. Mwanachama ambaye ana hisa nyingi zaidi ni hisa 581 zenye thamani ya shilling 5,810,000/= ambazo hazizidi 20% ya hisa zote kulinganana sheria ya ushirika.

MIPANGO YA MAENDELEO YA BAADAYE

SACCOS itaendelea na mpango wa kuboresha na kuleta faida kwa njia ya kubuni huduma mbalimbali zenye manufaa kwa wanachama bila kutumia gharama kubwa na kwa kuzingatia hatari zinazoweza kujitokeza katika kuboresha shughulizi hizo. Mipango iliyopo ni kutekeleza maadhimio yaliyopo kwenye mpango mkakati wa miaka mitano 5 uliyopitishwa na wanachama kwenye mkutano mkuu wa mwaka pia bodi ina mpango wa kubuni na kuongeza bidhaa mpya.

MATOKEO YA SHUGULI ZA KIBIASHARA NA GAWIO

Katika mwaka huu SACCOS imepata faida ya shilingi 18,403,662/= ukilinganisha na mwaka uliopita faida iliyopatikana ilikuwa ni 15,821,010/= kabla ya tengo la kodi. Chama hakijatoa gawio kwa wanachama wake kwa sababu bado kinaendelea kujenga na kuimarisha mtaji wa ndani. Bodi ya chama ina mpango wa kuandaa na kupeleka agenda ya kulipa gawio kwa wanachama kwenye mkutano mkuu ujao.

HALI YA UTENDAJI KWA MWAKA HUU

Kulingana na taarifa ya hali ya kifedha pamoja na mapato na matumizi kwa mwaka ulioishia-31/12/2020, hali inaonyesha kuwa urejeshaji wa mikopo ya wanachama unaboreka na mtaji wa SACCOS unakua. Uwezo wa SACCOS kutoa mikopo kwa kutumia akiba za wanachama ni wa kuridhisha. SACCOS imekuwa haitegemei mikopo toka taasisi za kifedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanachama wake japo mahitaji ya mikopo yanakuwa mengi kuliko uwezo wa chama. Wanachama wanahamasishwa kuweka akiba na amana zaidi ili kujenga uwezo wa chama kutumia mtaji wake wa ndani kuondokana na changamoto ya maombi mengi ya mikopo.

UDHIBITI WA HATARI NA MIFUMO YA NDANI

Bodi inatambua na kukubali wajibu wa kudhibiti majanga na hatari pamoja na udhibiti wa mifumo ya ndani ya SACCOS.Ni kazi ya menejimenti kuhakikisha kuwa upo utoshelezi wa mifumo ya ndani ya udhibiti wa kifedha na ya shuguli za uendeshaji wa SACCOS na ni endelevu ili kuwa na uhakika kuhusiana na: Kulinda mali za SACCOS,uendeshaji wa shughuli kwa wakati na gharama ndogo,kufuata sheria na kanuni zinazohusika, uhakika wa utimilifu wa miamala ya kifedha na uwezo wa kuwa endelevu katika shughuli za SACCOS.

Bodi imetathmini udhibiti wa hatari na mifumo ya ndani kwa kupitia kamati ya usimamizi ya SACCOS na kubaini kuwa mifumo iliyopo inatosheleza isipokuwa chama kimeandaa sera mbalimbali ikiwemo sera ya udhibiti majanga.

HALI YA UHAI WA SACCOS

Bodi inathibitisha kuwa kanuni za uhasibu zimefuatwa katika kutayarisha hesabu hizi na katika hali ya uhai endelevu wa SACCOS.Bodi ina kila uthibitisho kuwa shughuli za SACCOS zitakuwa na uhai endelevu kwa miaka ijayo.

HUDUMA KWA WATUMISHI

Mahusiano kati ya menejimenti na bodi

Kumekuwepo na mahusiano mazuri kati ya menejimenti, bodi na wadau wengine katika mwaka huu. Hapakuwepo na migogoro yoyote ambayo haikutatuliwa na

kumekuwepo na hali ya amani na mahusiano mazuri kwa watumishi na bodi. SACCOS haibagui watu katika kutoa nafasi za ajira kwani kila raia mwenye sifa anaweza kuajiriwa bila kujali jinsia, dini, kabila na ulemevu.

MAFUNZO

Kwenye bajeti inayoishia Desemba 31, 2020, jumla ya shilingi 20,707,500/= zikijumuisha mafunzo ya ndani na nje ya nchi zilitengwa kwa ajili ya mafunzo mbalimbali ya watendaji, bodi na wanachama.

HUDUMA ZA MATIBABU

Bodi ya chama kupia sera ya utumishi imeanza kutoa huduma za matibabu kwa watendaji wake kupitia mfuko wa taifa wa bima ya afya NHIF.

HALI YA USALAMA NA AFYA

Mazingira ya SACCOS yanahakikishwa kuwa yapo katika hali ya usalama na kiafya kwa watumishi kwa ujumla.

MPANGO WA MAFAO KWA WATUMISHI

Kwa sasa chama kimeajiri watumishi watatu, meneja na maafisa mikopo wawili wote ni waajiriwa wa mikataba ya miaka mitatu mitatu, pamoja na makato ya mishahara kwa watumishi SACCOS inawachangia watumishi katika mfuko wa hifadhi ya jamii NSSF kwa kiwango cha asilimia 10% ya mishahara yao.

JINSI (ME/KE) ZA WATUMISHI

SACCOS Ina watumishi watatu, wakiume wawili na wakike mmoja.

MICHANGO YA HIARI KWA VYAMA VYA KISIASA NA KIJAMII

LESA SACCOS haikutoa mchango wowote Kwenye kundi la kijamii kwa mwaka 2020 kutokana na changamoto za ugonjwa wa Corona (COVID - 19).

WAJIBU WA BODI

Sheria ya ushirika inazitaka bodi za vyama kuhakikisha kuwa hesabu za SACCOS zinatayarishwa kwa kuonyesha hali halisi yake ya kifedha na kifaida au hasara kwa kila mwaka wa fedha.Pia inazitaka bodi kuhakikisha kuwa vitabu vinaandikwa kulingana na miongozo ya uhasibu iliyopo na kuonyesha hali halisi ya kifedha ya SACCOS. Bodi inalo jukumu pia la kuhakikisha kuwa mali za chama zinalindwa na hakuna ubadhirifu wowote unaotokea katika mali za SACCOS.

Bodi inakubali jukumu hili na kubainisha kuwa hesabu hizi zimeandaliwa kwa kufuata miongozo ya uhasibu iliyopo sasa kama inavyotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA) ambayo ni IFRS.

WAKAGUZI

COASCO wamekuwa wakiteuliwa kuwa wakaguzi wetu, na wameonesha nia ya kuendelea kuwa wakaguzi wa SACCOS yetu.

UTHIBITISHO

Imeidhinishwa na Bodi ya SACCOS tarehe---22/07/2021------ na kusainiwa kwa niaba ya bodi na:

....
Ndg. EVA BOSCO
MWENYEKITI WA BODI

....
Ndg. DEONATUS KIHEKA
KATIBU WA BODI

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY
P.O Box 75...
22 JUL 2021
KINONDONI
★ DAR ES SALAAM ★

TAMKO LA MKUU WA FEDHA/AKAUNTI WA LESA SACCOS LTD

Mimi **DEONATUS KIHEKA** nikiwa na mamlaka ya mhasibu wa **LESA SACCOS LTD**, nakiri wajibu wangu wa kuhakikisha kuwa hesabu za chama kwa mwaka ulioishia tarehe 31.12.2020 zimeandaliwa kulingana na sharia husika za kihasibu na matakwa mengineyo ya kisheria.

Ninathibitisha kuwa hesabu za chama zinaonesha hali halisi ya fedha na matokeo ya shughuli zake mnamo tarehe hiyo na zimetayarishwa kupitia nyaraka za kifedha zilizorekodiwa na kuhifadhiwa vizuri.

Sahihi: ....

Nafasi: **Mkuu wa fedha**

NBAA Na: **4071**

Tarehe: 22/07/2021

TAARIFA HURU YA MKAGUZI KWAWANACHAMA WA CHAMA CHA USHIRIKA LESA SACCOS LTD

Ripoti Inayohusu Taarifa za Fedha Kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 31.12.2020

Hati Inayoridhisha

Tumekagua taarifa za fedha za **LESA SACCOS Ltd,** ambazo zinajumuisha taarifa ya hali ya fedha ya tarehe 31 Disemba, 2020, na taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya mabadiliko ya mtaji na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, na maelezo ya ufafanuzi wa taarifa za fedha, kujumuisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu.

Kwa maoni yetu, taarifa za fedha zilizoambatanishwa zinaonesha hali halisi ya fedha ya Chama cha Ushirika ya tarehe 31 Disemba, 2020, na matokeo ya shughuli zake pamoja na mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha.

Msingi wa Maoni

Ukaguzi wetu ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa. Wajibu wetu chini ya hivyo viwango umeelezwa katika aya ya wajibu wa mkaguzi kwa taarifa za fedha ya taarifa yetu. Tuko huru kulingana na matakwa ya maadili yanayohusiana na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha Tanzania, na tumetimiza wajibu wetu mwingine wa maadili kulingana na matakwa haya. Tunaamini ushahidi wa ukaguzi ambao tumeupata unatosheleza na unafaa kwa ajili ya msingi wa hati inayoridhisha.

Jambo la Msisitizo

1. Tunatoa msisitizo katika jedwali Na. 12 la taarifa hizi za fedha linalooonesha kwamba kunako tarehe 31 Disemba, 2020 uwiano uliopatikana wa 1% wa mtaji wa taasisi ambao upo chini ya uwiano unaotakiwa wa 6% kama inavyoelekezwa na kanuni ya 18 ya Kanuni za Taasisi ndogo ndogo za fedha (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo) za mwaka 2019.

Mambo Muhimu ya Ukaguzi

Mambo muhimu ya ukaguzi ni yale kwa ukadirifu wa taaluma yalikuwa muhimu zaidi katika ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka huu. Mambo haya yalielezwa katika muktadha wa ukaguzi wetu wa taarifa za fedha kwa ujumla, na katika kutoa maoni yetu juu yake, hatutoi maoni tofauti katika mambo haya.

Taarifa Nyingine

Uongozi wa Chama unawajibika kwa ajili ya taarifa nyingine. Taarifa nyingine ni pamoja na taarifa ya Wajumbe wa Bodi na Tamko la Mkuu wa Idara ya Fedha lakini hazijumuishi taarifa za fedha na taarifa yetu ya ukaguzi.

Maoni yetu juu ya taarifa za fedha hayahusishi taarifa nyingine na hatutoi uthibitisho wa aina yoyote juu yake. Ukiunganisha na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha, wajibu wetu ni kusoma taarifa nyingine na kwa kufanya hivyo, tunaangalia kama taarifa nyingine kwa kiasi kikubwa haziendani na taarifa za fedha au uelewa wetu tulioupata wakati wa ukaguzi, ama vinginevyo zinaonekana kupotoshwa.

Iwapo, kutokana na kazi tuliyoifanya kuhusu taarifa nyingine itabainika kwamba kuna upotoshaji wa taarifa hizi nyingine, tunatakiwa kutoa taarifa juu ya ukweli huo. Hatuna jambo la kutolea taarifa kuhusu suala hili.

Wajibu wa Bodi ya Chama cha Ushirika

Bodi ya Chama cha Ushirika inawajibu wa kutayarisha na kuwasilisha taarifa hizi za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013. Vilevile bodi inawajibu wa kuweka mfumo wa udhibiti wa ndani ambao bodi inaona ni muhimu katika kutayarisha taarifa za fedha ambazo hazina dosari kubwa zinazotokana na udanganyifu au makosa ya kawaida.

Katika kutayarisha taarifa za fedha bodi inawajibu wa kutathmini uwezo wa Chama kuwa endelevu, ikionesha, kadri inavyofaa, mambo yanayohusiana na Chama kuwa endelevu na kutumia msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu isipokuwa ama bodi inakusudia kukifilisi Chama au kusitisha shughuli au hakina njia mbadala ya kweli isipokuwa kufanya hivyo.

Wajibu wa Mkaguzi

Shabaha yetu ni kupata uhakika wa maana kama taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina upotoshaji mkubwa, ama kwa sababu ya udanganyifu au makosa ya kawaida, na kutoa taarifa ya mkaguzi ambayo inajumuisha maoni yetu. Uhakika wa maana ni kiwango cha juu cha uhakika, lakini siyo dhamana kwamba ukaguzi uliofanyika kulingana na viwango vya ukaguzi vya kimataifa kila mara utagundua upotoshaji mkubwa unaokuwepo. Upotoshaji unaweza kutokana na udaganyifu au makosa ya kawaida na unafikiriwa kuwa mkubwa kama, peke yake au kwa ujumla, ungeweza kuathiri maamuzi ya watumiaji kwa msingi wa taarifa hizi za fedha.

Vilevile, kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 kinatutaka tujiridhishe kama shughuli za Chama cha Ushirika zimefanyika kulingana na matakwa ya Sheria au la na, kama vitabu na hesabu za Chama vina kubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama.

Kama sehemu ya ukaguzi kulingana na Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa, tunatumia maamuzi ya weledi na tunadumisha weledi kwa kushuku wakati wote wa ukaguzi. Pia:

- Tunatambua na kutathmini hatari za upotoshaji mkubwa wa taarifa za fedha, ama kutokana na udanganyifu au makosa ya kawaida, kupanga na kufanya ukaguzi kuitikia hatari hizo, na kupata ushahidi unaotosheleza na kufaa kwa ajili ya msingi wa maoni yetu. Hatari ya kutogundua upotoshaji mkubwa unaotokana na udanganyifu ni kubwa kuliko hatari inayotokana na makosa ya kawaida, kwa sababu udanganyifu unaweza kuhusisha njama, kughushi, kuondoa taarifa kwa makusudi, mawasilisho yasiyo sahihi, au kupuuza mfumo wa udhibiti wa ndani.

- Kupata ufahamu wa udhibiti wa ndani kuhusiana na ukaguzi ili kupanga njia za ukaguzi ambazo zinafaa, lakini siyo kwa makusudi ya kutoa maoni juu ya kufaa kwa udhibiti wa ndani wa Chama.

- Kutathmini kufaa kwa sera za uhasibu zinazotumika na usahihi wa makadirio ya uhasibu na maelezo bayana yaliyofanywa na uongozi.

- Kuhitimisha kufaa kwa matumizi ya bodi juu ya msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu na, kwa kuzingatia ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, ama kuwepo kwa mashaka makubwa kuhusiana na matukio au hali inayoweza kuleta mashaka makubwa juu ya uwezo wa Chama kuendelea kuwa endelevu. Kama tunahitimisha kwamba yapo mashaka makubwa, tunatakiwa kuvuta nadhari katika taarifa yetu ya ukaguzi kuhusiana na maelezo bayana katika taarifa za fedha au, kama maelezo hayo hayatoshelezi, tubadilishe maoni yetu. Hitimisho letu limejengwa juu ya ushahidi wa ukaguzi tulioupata hadi kufikia tarehe ya taarifa yetu ya ukaguzi. Hata hivyo, matukio au hali za siku za usoni zinaweza kusababisha Chama kukoma kuendelea kuwa endelevu.

Tunawasiliana na Bodi ya Chama cha Ushirika kuhusiana, miongoni mwa mambo mengine, mawanda yaliyopangwa na muda wa ukaguzi na matokeo makubwa ya ukaguzi, kujumuisha mapungufu yoyote makubwa katika udhibiti wa ndani ambayo tunayabaini wakati wa ukaguzi wetu.

Pia tunatoa taarifa kwa Bodi ya Chama cha Ushirika ya kwamba tumefuata matakwa ya miiko ya kuwa huru, na tunawasiliana nao kuhusu mahusiano na mambo mengine yote yanayoweza kufikiriwa kukiuka uhuru wetu na pale inapobidi jinsi ya kuulinda.

Ripoti Inayohusu Matakwa Mengine ya Kisheria na Usimamizi

Kulingana na matakwa ya kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, tunatoa taarifa kwa maoni yetu kwamba:

a) Vitabu vya hesabu vilivyotunzwa na Chama vinakubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama; na

b) Shughuli za Chama zimefanyika kulingana na madhumuni ya Chama, Masharti na maamuzi yaliyofanyika katika mkutano mkuu wa Chama.

SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)

CPA Z.E. MKINGULE
KAIMU MKURUGENZI MKUU

Barabara ya Hatibu
DODOMA
Tarehe: 20/07/2021

CO-OPERATIVE AUDIT & SUPERVISION CORPORATION
P. O. Box 761
DODOMA

Nakala kwa: Mrajis wa Vyama vya Ushirika
DODOMA

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika
DAR ES SALAAM

Afisa Ushirika (W)
KINONDONI

TAARIFA YA HALI YA FEDHA KUNAKO TAREHE 31.12.2020

		31.12.2020	31.12.2019
		TZS	TZS
MALI YA MUDA MREFU	**JED**		
Taslimu na Usawa	2	179,950,372	188,639,530
Mikopo kwa Wanachama	3	4,580,637,240	3,394,233,944
Bidhaa Mwishoni(Stock)		1,635,000	1,710,000
Kodi inayosubiliwa		1,526,185	1,989,032
Wadaiwa wengineo	4	143,181,681	141,375,948
Mali na vifaa	5	1,574,606	3,690,179
JUMLA YA MALI		**4,908,505,084**	**3,731,638,632**
MTAJI NA DHIMA			
MTAJI			
Akiba ya lazima		21,580,450	19,117,458
Akiba ya kukombolea mafungu		10,790,226	9,558,730
Akiba ya elimu		16,185,338	14,338,094
Akiba ya madeni mabaya		16,185,338	14,338,094
Limbikizo la ziada/Hasara		36,611,083	31,685,100
JUMLA YA MTAJI		**101,352,434**	**89,037,476**
DHIMA			
Hisa za Wanachama		311,180,036	207,890,036
Akiba za Wanachama		4,233,694,420	3,253,139,047
Wadai	6	262,278,195	181,572,072
JUMLA		**4,807,152,651**	**3,642,601,156**
JUMLA YA MTAJI NA DHIMA		**4,908,505,085**	**3,731,638,632**

JEDWALI 1 HADI 15 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

MWENYEKITI............................ **TAREHE** 22/07/2021

KATIBU...................................... **TAREHE** 22/07/2021

SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY P.O.Box 7833 22 JUL 2021 KINONDONI DAR ES SALAAM

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA, 2020

		2020 TSHS	2019 TSHS
MAPATO	**JED**		
Riba juu ya Mkopo		501,858,244	438,221,033
Toa: Gharama za Fedha	7	238,401,497	147,632,832
		263,456,747	290,588,201
Mapato mengineyo	8	11,591,813	19,133,916
		275,048,560	**309,722,117**
MATUMIZI			
Gharama za Watumishi	9	89,172,720	78,300,000
Gharama za Uendeshaji	10	167,472,179	215,601,107
JUMLA YA MATUMIZI		**256,644,899**	**293,901,107**
Ziada kabla ya Kodi		**18,403,662**	**15,821,010**
Kodi (30%)	11	6,088,704	2,757,271
Ziada baada ya Kodi		**12,314,958**	**13,063,739**

JEDWALI 1 HADI 15 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

MWENYEKITI.......................... **TAREHE** 22/07/2021

KATIBU.......................... **TAREHE** 22/07/2021

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY P.O.Box 78?? 22 JUL 2021 KINONDONI ★ DAR ES SALAAM ★

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2020

MAELEZO	AKIBA YA LAZIMA	AKIBA YA KUKOMBOLEA MAFUNGU	AKIBA YA ELIMU	AKIBA YA MADENI MABAYA	LIMBIKIZO LA ZIADA	JUMLA YA MTAJI
	20%	10%	15%	15%		
	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS
Salio anzia 01.01.2019	**16,504,711**	**8,252,356**	**12,378,533**	**12,378,533**	**26,459,604**	**75,973,737**
Ziada ya mwaka					13,063,739	13,063,739
Matengo kwa Mwaka	2,612,748	1,306,374	1,959,561	1,959,561	(7,838,243)	
Baki 31.12.2019	**19,117,459**	**9,558,730**	**14,338,094**	**14,338,094**	**31,685,100**	**89,037,476**
Salio anzia 01.01.2020	**19,117,459**	**9,558,730**	**14,338,094**	**14,338,094**	**31,685,100**	**89,037,476**
Ziada ya mwaka					12,314,958	12,314,958
Matengo kwa Mwaka	2,462,992	1,231,496	1,847,244	1,847,244	(7,388,975)	
Baki 31.12.2020	**21,580,450**	**10,790,226**	**16,185,338**	**16,185,338**	**36,611,083**	**101,352,434**

JEDWALI 1 HADI 15 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

MWENYEKITI.............................. TAREHE....22/07/2021

KATIBU.................................... TAREHE....22/07/2021

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY
P.O.Box 7833
22 JUL 2021
KINONDONI
DAR ES SALAAM

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA KUISHIA TAREHE 31.12.2020

	31.12.2020 TZS	31.12.2019 TZS
Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji		
Ziada kabla ya kodi	12,314,958	15,821,010
Uchakavu	3,434,841	3,465,505
Jumla	**15,749,798**	**19,286,515**
Mabadiliko ya Mtaji Uzungukao:		
(Ongezeko)/Punguzo la Mikopo ya Wanachama	(1,186,403,296)	(586,912,941)
Ongezeko/(Punguzo) la Akiba za Wanachama	980,555,373	591,891,575
Ongezeko/(punguzo) la Hisa za Wanachama	103,290,000	37,370,026
Ongezeko/Punguzo kwa bidhaa mwishoni	75,000	(1,710,000)
Ongezeko/Punguzo la kodi iliyoahilishwa	462,847	(1,224,735)
Ongezeko/(punguzo) la Wadaiwa	(1,805,733)	(26,626,499)
Ongezeko/(punguzo) la Wadai	80,706,123	(23,878,853)
Jumla	**(24,438,955)**	**(11,091,427)**
Fedha halisi kutokana na shughuli za Uendeshaji	**(8,689,157)**	**8,195,088**
Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji		
Ongezeko la Mali za Kudumu	-	-
Fedha halisi kutokana na shughuli za Uwekezaji	**-**	**-**
Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha	-	-
Fedha halisi kutokana na shughuli za Fedha		
Fedha Mwanzoni mwa mwaka	188,639,530	8,195,089
Kuongezeka/(Kupungua) kwa fedha	(8,689,157)	180,444,441
Fedha mwisho wa mwaka	**179,950,373**	**188,639,530**

JEDWALI 1 HADI 15 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

MWENYEKITI.............................. **TAREHE** 22/07/2021

KATIBU.............................. **TAREHE** 22/07/2021

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY P.O.Box 7833 22 JUL 2021 KINONDONI DAR ES SALAAM

JEDWALI ZA HESABU KUISHIA TAREHE 31.12.2020

JEDWALI NA. 1.

1. MAELEZO YA JUMLA

LESA SACCOS Ltd kimeandikishwa mnamo tarehe 7/02/2011 chini ya sheria ya mwaka 2003, nambari ya kuandikishwa ni DSR 1299 Chama hiki kipo katika Manispaa ya Kinondoni Tanzania.

1.1. MUHTASARI WA SERA MUHIMU ZA UHASIBU

1.1.2 Maandalizi ya Msingi

Taarifa hizi za fedha za LESA savings and Credit Co-operative Society Limited zimetayarishwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha (IFRS). Taarifa za fedha zimetayarishwa chini ya mkataba wa gharama wa kihistoria.

Hakuna marekebisho yaliyofanywa kwa vipengele vya mfumko wa bei vinavyoathiri hesabu.

1.1.3 Taarifa Za Ufuatiliaji Wa Viwango Vya Kimataifa Vya Utoaji Taaarifa Za Fedha

Taarifa za fedha zimetayarishwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya utoaji Taarifa za Fedha (IFRSs) na tafsiri yake iliyopitishwa na Bodi ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IASB).

1.1.4. Fedha tasilimu na Ulinganifu wa Fedha

Fedha tasilimu na thamani ya fedha huendelezwa kwenye mizania katika thamani iliyoandikwa kwa madhumuni ya taarifa ya mapato halisi, fedha taslimu na thamani ya fedha hujumuisha fedha zilizopo, amana zinazoshughulikiwa na amana za kudumu.

1.1.5. Utambuzi wa Mapato

Mapato hutambuliwa kwa kiasi kwamba inawezekana manufaa kiuchumi yataingia kwenye chama na mapato kuweza kupimwa kwa uhakika. Vigezo maalum vya utambuzi vifuatavyo lazima vifikiwe pia kabla ya kuyatambua mapato.

- Faida itokanayo na mikopo iliyotolewa hutambuliwa katika taarifa ya mapato kwa kuzingatia fedha iliyopokelewa kipindi cha mwaka wa fedha.
- Mapato mengineyo mfano viingilio hutambuliwa katika taarifa ya mapato kwa kuzingatia fedha.

1.2. Kipindi cha Hesabu

Chama huandaa hesabu zake kwa muda wa miezi 12 kuishia tarehe 31 Desemba.

1.2.1. Faida juu ya Mikopo

Kiwango cha faida juu ya mikopo ni asilimia 16% ya mkopo toka kwa mwanachama.

1.2.2. Sera ya Matengo

Matengo toka ziada iliyopatikana yamewekwa kwa kuzingatia Kanuni Na. 67 a,b, na c kama ifuatavyo:-

- Akiba ya Lazima - 20%
- Akiba ya Kukombolea Mafungu - 15%
- Akiba ya Madeni Mabaya - 15%
- Akiba ya Elimu - 10%

2. MGAO WA ZIADA

Mgao utatengwa kwa wanachama baada ya hesabu za chama kukaguliwa pia kuondoa matengo yote ya kisheria kama ilivyoainishwa kwenye masharti ya chama. Mgao lazima uwe umeidhinishwa na Mkutano Mkuu na kupitishwa na Mrajis wa Ushirika.

JEDWALI LA HESABU KUISHIA 31.12.2020

		31.12.2020 TSHS	31.12.2019 TSHS
JED.2	**TASLIM NA USAWA**		
	Fedha Benki NMB	137,170,118	145,587,889
	Fedha Benki CRDB	42,780,254	43,051,641
	JUMLA	**179,950,372**	**188,639,530**
JED. 3	**MIKOPO KWA WANACHAMA**		
	Mikopo kwa Wanachama	4,583,963,784	3,395,183,926
	Tengo la madeni mabaya	(3,326,544)	(949,982)
	JUMLA	**4,580,637,240**	**3,394,233,944**
JED. 4	**WADAIWA**		
	Wadaiwa wengineo (Mwajiri)	143,181,681	141,375,948
	JUMLA	**143,181,681**	**141,375,948**
JED.6	**WADAI**		
	COASCO	3,000,000	3,000,000
	Wadai wengineo(Mrajis 2020)	5,291,182	16,809,780
	Riba juu akiba	214,561,347	147,632,832
	Kodi ya Zuio	40,243,798	16,403,648
	Kodi ya Mapato (TRA)	(818,132)	(2,274,188)
	JUMLA	**262,278,195**	**181,572,072**

		2020 TSHS	2019 TSHS
JED. 7	**GHARAMA ZA FEDHA**		
	Riba juu ya akiba	238,401,497	147,632,832
	JUMLA	**238,401,497**	**147,632,832**

JEDWALI LA HESABU KUISHIA 31.12.2020

		31.12.2020 TSHS	31.12.2019 TSHS
JED. 8	**MAPATO MENGINEYO**		
	Viingilio	1,440,000	3,750,000
	Ushuru wa Bima(Mfuko wa ndani)	10,076,813	13,093,916
	Mauzo ya Tshirt	75,000	2,290,000
	JUMLA	**11,591,813**	**19,133,916**
JED. 9	**GHARAMA ZA UTUMISHI**		
	Mishahara na ujira watendaji	82,595,520	72,036,000
	NSSF	6,577,200	6,264,000
	JUMLA	**89,172,720**	**78,300,000**
JED. 10	**GHARAMA ZA UENDESHAJI**		
	Pango la Ofisi	2,400,000	2,400,000
	Ada ya Ukaguzi	3,000,000	3,000,000
	Gharama za Benki	3,067,194	1,594,522
	Posho za Wajumbe- Bodi na Kamati	37,200,000	44,106,000
	Gharaza za Uchakavu	3,434,841	3,465,505
	Mfuko wa Mrajis	2,000,000	2,000,000
	Maji na Umeme	750,000	1,980,000
	Mawasiliano na Usafiri	2,626,500	4,155,900
	Posho za Safari Mafunzo	10,430,000	9,580,000
	Mafunzo na Elimu	11,210,000	4,782,000
	Shajala	1,575,300	409,350
	Gharama za Mkutano Mkuu	77,140,000	103,402,000
	Kodi ya zuio	-	16,403,648
	Ongezeko tengo la madeni mabaya	2,376,562	949,982
	Gharama za kuandaa Mpango mkakati	-	3,050,000
	Mchango kwa Jamii (CSR)	-	358,000
	Gharama za kutengeneza T-shirt	-	3,626,000
	Tengo la elimu Mrajis (2021)	3,291,182	5,293,200
	NHIF bima kwa wafanyakazi	4,503,600	3,900,000
	Matumizi mengineyo	2,467,000	1,145,000
	JUMLA	**167,472,179**	**215,601,107**

JED. 11	GHARAMA ZA KODI		
	(i) Kodi Mpya		
	Ziada kabla ya kodi	18,403,662	15,821,010
	Add: Makato yasiyokubalika		
	Uchakavu	3,434,841	3,465,505
		21,838,502	**19,286,515**
	Less: Makato yanayokubalika		
	Upungufu wa thamani	-	3,465,505
		21,838,502	**15,821,010**
	Kodi ya mapato 30%	6,551,551	4,746,303
	(ii) Kodi inayosubiliwa		
	Kodi subiliwa iliyorejeshwa	(462,847)	(1,989,032)
	Gharama za kodi	**6,088,704**	**2,757,271**
	Salio anzia 1 Januari 2019	(2,274,188)	(230,856)
	Ongezeko	6,088,704	2,757,271
	Less: Malipo ya kodi kwa mwaka	(4,632,648)	(4,800,603)
	Salio ishia 31 Desemba 2020	**(818,132)**	**(2,274,188)**

JED:12	MTAJI TETE		
	Hisa za wanachama	311,180,036	207,890,036
	Akiba ya Lazima	21,580,450	19,117,458
	Limbikizo la ziada	36,611,083	31,685,100
	JUMLA	**369,371,569**	**258,692,594**
	MALI		
	Taslimu na Usawa	179,950,372	188,639,530
	Mikopo kwa Wanachama	4,580,637,240	3,394,233,944
	Bidhaa Mwishoni(Stock)	1,635,000	1,710,000
	Kodi inayosubiliwa	1,526,185	1,989,032
	Wadaiwa wengineo	143,181,681	141,375,948
	Mali na vifaa	1,574,606	3,690,179
	JUMLA	**4,908,505,084**	**3,731,638,633**
	Uwiano wa chini unaokubalika	%	%
	Mtaji tete(>8%)	8	7
	Mtaji halisi(>6%)	1	1

JED. 13 DHIMA ISIYOIVA:

Uongozi wa chama umethibitisha kuwa hapakuwepo na kesi yoyote kunako tarehe ya mizania.

JED.14 MRADI ENDELEVU:

Uongozi wa chama umethibitisha kuwa hapakuwepo na mikataba yoyote kwa ajili ya ujenzi/ununuzi wa mali za kudumu hadi tarehe ya mizania.

JED. 15 MALINGANISHO YA HESABU

Malinganisho ya hesabu ya mwaka uliopita yamezingatia taarifa ya mwaka huu hivyo kuzifanya zilingane

JEDWALI LA MALI YA KUDUMU KUNAKO 31 DECEMBER,2020

JED. NO 5 MALI NA VIFAA VYA KUDUMU

MALI	BEI	ONGEZEKO	BEI	LIMBIKIZO LA UCHAKAVU	KIWANGO	TOZO KWA MWAKA	LIMBIKIZO LA UCHAKAVU	BAKI HALISI VITABUNI TZS	BAKI HALISI VITABUNI TZS
	TZS	TZS	TZS	TZS	%	TZS	TZS	TZS	TZS
	1.1.2020		31.12.2020	1.1.2020			31.12.2020	31.12.2020	31.12.2019
Samani	5,385,106	-	5,385,106	3,182,290	12.5%	673,138	3,855,428	1,529,678	2,202,816
Mfumo laini(CRDB Finance Solution)	5,000,000		5,000,000	4,999,999	33.3%	1	4,999,999	1	1
Accounting Software(Saccos Plus)	8,260,000	-	8,260,000	5,501,160	33.3%	2,750,580	8,251,740	8,260	1,383,550
Komputa(2)	6,399,000		6,399,000	1	33.3%	1	6,398,999	1	1
Kitunza taarifa(Server)	7,501,900		7,501,900	1	33.3%	1	7,501,899	1	1
Printer	35,633		35,633	1	12.5%	1	35,632	1	1
Kasiki	103,805		103,805	58,599	5.0%	5,190	67,146	36,659	103,805
Kihifadhi Umeme(UPS-APC) 2	451,580		451,580	1	12.5%	1	451,579	1	1
Kihifadhi Maji(Water dispenser)	42,969		42,969	1	12.5%	1	42,968	1	1
Kabati (File Cabinet)	205,401		205,401	1	12.5%	5,924	205,400	1	1
Komputa(Laptop)	213,425		213,425	1	33.3%	1	213,424	1	1
Printer	182,813		182,813	1	12.5%	1	182,812	1	1
JUMLA 31.12.2020	**33,781,632**	-	**33,781,632**	**13,742,056**	-	**3,434,841**	**32,207,026**	**1,574,606**	**3,690,179**
JUMLA 31.12.2019	**33,848,808**	-	**33,848,808**	**23,117,109**	-	**3,465,505**	**30,158,629**	**3,690,179**	-